

# Mwongozo Uliosasishwa: Nakala ya Kutembelea Wapendwa Wako katika Utunzaji wa Muda Mrefu

[muziki unaocheza]

*[Ujumbe Kwenye Skrini] Mwongozo Uliosasishwa: Kutembelea Wapendwa walio katika Utunzaji wa Muda Mrefu*

[Maria] Hujambo, jina langu ni Maria na ninafanya kazi na Idara ya Afya ya Minnesota.

Hivi punde nitaupitia na wewe mwongozo kuhusu kutembelea, na hata kukumbatiwa, na wapendwa wanaoishi katika vituo vya utunzaji wa muda mrefu.

Chanjo za COVID-19 na kupungua kwa kasi ya maambukizi kunaleta uwezekano wa kuongeza ziara salama zinazoleta pamoja wakazi wa utunzaji wa muda mrefu na familia zao na marafiki.

*[Ujumbe kwenye Skrini] Ili kujifunza kuhusu maelezo yaliyosasishwa kuhusu jinsi na wakati gani unaweza kumtembelea mpPENDWA WAKO, piga simu kwa makazi yao.*

[Maria] Ili kujifunza kuhusu maelezo yaliyosasishwa kuhusu jinsi na wakati gani unaweza kumtembelea mpPENDWA WAKO, piga simu kwa makazi yao.

Wakazi wa utunzaji wa muda mrefu sasa wanaweza kukusanyika na wengine na wakazi ambao wamepewa chanjo kamili wanaweza kukumbatia wageni wao. Wakazi na wageni wao watahitaji kuva barakoa na kuhakikisha wananaawa mikono kabla na baada ya kutembeleana.

Ingawa matembezi ya ndani yanaruhusiwa, matembezi ya nje bado yanapendelewa, inapowezekana, kwa sababu kwa ujumla kuna hatari ndogo ya kueneza COVID-19.

Uwezo wa kituo cha utunzaji wa muda mrefu kuwa na wageni unaweza kubadilika kwa hivyo wageni wanapaswa kupiga simu kabla ya kuzuru kwao ili wapate maelezo zaidi.

*[Nembo ya MN ya Kukaa Salama na kiungo cha <https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/hcp/ltc.html>]*

[muziki unaochangamsha]

Minnesota Department of Health  
Communications Office  
PO Box 64975  
St. Paul, MN 55164-0975  
651-201-4989  
[health.communications@state.mn.us](mailto:health.communications@state.mn.us)  
[www.health.state.mn.us](http://www.health.state.mn.us)

3/30/21 (Swahili)

*Ili kupata maelezo haya katika muundo tofauti, piga simu kwa: 651-201-4989 651-201-4989*